The Olkaria II 64MW Geothermal Power Project was commissioned in November 2003. This Project will inject additional 64MW into the grid.

##### Sondu Miriu 60MW Hydro Power Project

Construction work on the project continued to be adversely affected by



the suspension of funds by the project lenders due to environmental and social impact issues, which are being addressed by the concerned stakeholders. The project includes a 50 km 132kV transmission line from the power station to the Company's Kisumu 132/33kV sub-station.

### FUTURE OUTLOOK

For the last four years, the trading performance of your Company was adversely affected by lack of adequate generation capacity, high cost of bulk electricity purchases and a depressed economy where real GDP growth was -0.3% in 2000, 1.1% in 2001 and 0.9% in 2002.

Currently, there is adequate generation capacity to meet present demand while implementation of the committed generation projects will secure future demand. As the measures implemented so far have already started showing positive results, coupled with projected recovery of the economy where GDP is expected to grow by 1.4% in 2003, directors are optimistic about prospects of your Company returning to profitability in the current financial year.

### CONCLUSION

I wish to thank my colleagues in the Board and staff for their hard work and commitment to our strategic recovery initiatives during a period when the Company operated under a very challenging environment. On behalf of your Board, I would also like to thank the Government and KenGen for the tremendous support extended to your Company during the year, which will aid in the recovery process.

ENG. ALFRED SAMBU  
CHAIRMAN

# TATHMINI KUTOKA KWA MWENYEKITI



Eng. Alfred Sambu

## TATHMINI KWA UJUMLA

Mikakati ya harakati iliyoanzishwa mnamo 2001/02 kuirejesha Kampuni yenu katika hali ya utengezaji wa faida iliendelea kutiliwa mkazo katika shughuli za Kampuni hii katika kipindi hiki cha mwaka ninachokifanyia tathmini, ingawa sio kwa kasi kutokana na kuwepo kwa mashauriano yaliyostahili kwa pamoja na washika dau wahusika, ambayo yaliathiriwa na kuingia kwa serikali mpya mnamo Desemba, 2002. Hata hivyo nina fahari kusema kwamba licha ya mikabala migumu katika utekelezaji kazi, mafanikio ya kimsingi yalipatikana ambayo yalikuwa na athari nzuri katika tendakazi za Kampuni hii mwanzoni mwa mwaka huu wa matumizi ya fedha. Kwa muktadha huo basi, usawazishaji wa kiwango kikubwa cha ushuru kwa pamoja na Kampuni yetu tanzu ya utoaji nguvu za umeme ya KenGen ulikamilishwa na kuidhinishwa na kuidhinishwa na serikali mnamo mwezi Septemba, 2003. Hilo linatarajiwa litapunguza gharama za huduma za umeme kwa kiwango kikubwa na hivyo kuimarisha viwango vya kibiashara vya Kampuni hii, ambavyo vilizorota sana tangu mwaka wa 1999.

Katika shughuli nyingine kama hiyo, makubaliano ya kimsingi kwa pamoja na Kampuni ya KenGen na serikali, kwa ajili ya kulipa deni la Shilingi Milioni 12, 260 lililokuwa likidaiwa na

Kampuni hiyo, yaliafikiwa, kufikia tarehe 30 Juni, 2003, na serikali nayo kwa upande wake kulipwa kima cha shilingi Milioni 3,369 za hisa zisizokuwa na malimbikizi zikiwa na kiwango cha riba cha asilimia 4. Pamoja na hayo muwiano mpya wa hesabu za gharama na matumizi utawezesha kuwekwa kwa akiba ya kutajika katika kugharamia matumizi.

Hatua zingine za kimipango zilizokusudiwa kuirejesha Kampuni yenu katika hali ya utengezaji faida ambayo tayari imewasilishwa kwa washika dau ikiwa ni pamoja na uwezo wa upatikanaji wa nguvu za umeme za kutosha, kuchunguzwa na kusawazishwa kwa viwango vikubwa vya ushuru, kupunguzwa kwa viwango vya hasara, kuimarishwa kwa misingi ya kuwahudumia wateja na kugharamia shughuli za marekebisho, kuhakikisha kuna idadi ifaayo ya wafanyakazi, kuimarishwa kwa mtandao na kuimarishwa kwa utoaji wa huduma bora - ni mambo ambayo yanashughulikiwa kikamilifu kupitia kufanuliwa upya pamoja na kuzingatwa zaidi kwa yale ambayo yanaweza kuleta matokeo bora haraka. Halmashauri imenuia kuendeleza

mbele ufanisi ambao tayari umepatikana kufikia sasa ili kuhakikisha uimarishaji wa tendakazi katika kampuni yenu unapatikana katika kipindi hiki cha mwaka cha matumizi ya fedha.

## MATOKEO YA SHUGHULI ZA KIFEDHA

### Matokeo ya Kibiashara

Mapato kutokana na utoaji wa huduma za nguvu za umeme wakati wa kipindi hiki cha mwaka cha matumizi ya fedha yaliongezeka hadi Shilingi milioni 19,185 kutoka Shilingi milioni 18,699 zilizopatikana katika kipindi cha mwaka kilichotangulia, ikiwa ni nyongeza ya pato ya Shilingi milioni 486. Nyongeza hiyo ilitokana na kuongezeka kwa mauzo pamoja na kuimarika kwa ubora wa tendakazi. Kiwango cha kupunguza gharama ya utumizi wa mafuta ya petroli kilipungua kutoka Shilingi milioni 6,108 mwaka uliotangulia hadi Shilingi milioni 3,945. Hii ilitokana na kupunguzwa kwa utoaji wa umeme kutoka kwa nguvu za ardhi kutokana na kuimarishwa kwa utoaji wa kawi hiyo kutoka kwa nguvu za maji.



Forging partnerships with financiers from the East African Development Bank

Mapato mengine yalipungua kwa Shilingi milioni 439 kutoka Shilingi milioni 2,545 hadi Shilingi milioni 2,106 hasa hasa kutokana na kiwango cha chini cha mapato kutokana na kuachwa kwa utumizi wa rasilimali zisizokuwa za kimsingi ikilinganishwa na mwaka uliotangulia.

Gharama za ununuzi wa umeme usiotokana na utumizi wa mafuta ya petroli zilipanda kwa Shilingi milioni 798 hadi Shilingi milioni 14,513 kutoka Shilingi milioni 13,715 mwaka uliotangulia hasa kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha umeme kilichonunuliwa.

Gharama ya mafuta ya petroli ilipungua kwa Shilingi milioni 2,804 hadi Shilingi milioni 4,270 kutoka Shilingi milioni 7,074 mwaka uliotangulia. Hali hiyo ilitokana na kupunguzwa kwa utoaji wa umeme kutokana na nguvu za joto, kutokana na kuimarishwa kwa utoaji kutokana na nguvu za maji. Hata hivyo mapato yaliyopatikana kutokana na hilo ni ya kupunguza gharama na hayamo katika mapato ya jumla ya Kampuni.

Gharama ya usambazaji ilifikia Shilingi milioni 9,182 million. Hii inalinganishwa na Shilingi milioni 8,135 zilizotumika mwaka uliotangulia kabla ya kupatikana kwa gharama za uimarishaji upya kwa Shilingi milioni 978.

Ongezeko hilo la gharama lilitokana na ongezeko la gharama ya malipo kwa waliostaafu (Shilingi milioni 527), madeni yasiyolipwa (Shilingi milioni 232) na kupungua kwa thamani (Shilingi milioni 469) zaidi ya ilivyokuwa mwaka uliotangulia.

Kiwango cha jumla cha gharama ya tendakazi kabla ya gharama za uimarishaji upya kilipungua kwa asilimia 3 kutoka Shilingi milioni 28,924 katika mwaka uliotangulia hadi Shilingi milioni 27,965 Gharama hiyo ya chini ya tendakazi ilitokana na kupunguzwa kwa gharama ya mafuta ya petroli na wafanyakazi.

Gharama za kifedha ziliongezeka kutoka Shilingi milioni 300 katika mwaka uliotangulia hadi Shilingi milioni 1,384 kutokana na kiwango cha riba cha deni la Kampuni ya KenGen cha Shilingi milioni 660 na malimbikizi ya mikopo ya serikali ya Kenya ya Shilingi milioni 441.

Hasara kabla ya ushuru kwa hivyo iliongezeka kwa Shilingi milioni 1,263 kutoka Shilingi milioni 2,849 katika mwaka uliotangulia hadi Shilingi milioni 4,112 -.

#### Ushuru

Kutokana na hasara ya kibiashara iliyopatikana katika kipindi hiki, na baada ya kuongeza kiwango cha mkopo wa kugharamia ushuru cha Shilingi milioni 1,215 Kampuni ilikuwa na kiwango cha jumla cha hasara cha Shilingi milioni 2,897 ikilinganishwa na kiwango cha Shilingi milioni 1,879 mwaka uliotangulia.

#### Mgao wa Hisa

Kutokana na matokeo ya kibiashara yasiyondhisha, Wakurugenzi hawapendekezi mgao wa hisa katika hisa za kawaida za mwaka.

#### MIKAKATI NA MIPANGO YA UFUFUZI

Wana-Halmashauri na wasimamizi wa Kampuni kwa ushirikiano na washika dau wanaohusika wamefafanua upya mipango unayokusudiwa kutekelezwa kwa ajili ya kuigeuza Kampuni iwe katika hali ya utengezaji faida zaidi kwa muda mfupi zaidi iwezekanavyo. Hatua hizi zinalinga mikabala muhimu ambayo imechangia pakubwa katika matokeo ya kibiashara ya Kampuni hii, na kama zikifaulu hatua hizo basi kutakuwa na matokeo ya kuridhisha.

Hatua hizo zinaambatanisha kujishauri kuhusu kiwango cha juu cha ushuru kati ya Kampuni na watoaji wa vifaa vya umeme, kupunguzwa kwa hasara ya kimfumo, kuimarishwa kwa



*Transformer quality inspection*

misingi ya utoaji wa huduma kwa wateja, kuimarishwa kwa utoaji wa nguvu za umeme na kufanywa upya kwa mfumo wa wa kifedha.

#### Kuchunguzwa kwa bei ya jumla ya umeme

Kampuni iliendelea kufanya mashauri kuhusu kupunguzwa kwa bei ya jumla ya umeme na watoaji wakuu wa umeme ikiwa ni pamoja na Kampuni za KenGen, OrPower4 Inc., Westmont Power na Iberafrica. Mashauriano na Kampuni ya KenGen yalipelekea kupunguzwa kwa ushuru kwa kima cha KSh.0.60 kwa kWh kuanzia tarehe 1 Julai, 2003, ambacho kimeidhinishwa na serikali na kinasubiri idhinisho kutoka kwa Halmashauri inayosimamia utoaji wa umeme. Hatua hiyo inatarajiwa kupunguza kiwango cha jumla cha gharama ya ununuzi wa umeme kwa takriban Shilingi milioni 2,250 kwa mwaka. Mashauriano na watoaji hao wengine watatu wakuu yangali yanaendelea na inatarajiwa kwamba yatakamilishwa katika kipindi hiki cha mwaka cha matumizi ya fedha.

## Kupunguza Hasara Kupitia Urekebishaji Wa Vifaa

Wakati wa kipindi hiki cha mwaka hasara zilipungua kwa asilimia 0.52 kutoka asilimia 20.5 katika kipindi cha mwaka 2001/02 hadi asilimia 19.98 katika kipindi cha mwaka 2002/03.


Kampuni inachukua hatua za kuimarisha mifumo ya kupunguza hasara kwa kiwango cha asilimia 3 katika kipindi cha mwaka 2003/04, asilimia 1.5 katika kipindi cha mwaka 2004/05 na asilimia 1 kwa mwaka baada ya hapo.

Kwa kuafikia lengo hilo, kundi maalumu la kutekeleza hatua hizo limebuniwa ili kushughulikia kwa kina ushirikishaji na utekelezaji wa harakati zilizotambuliwa, ambazo ni pamoja na kuimarishwa kwa vituo vya ukaguzi wa utoaji wa huduma kwa wateja, utekelezaji wa mifumo ya uimarishaji wa tendakazi, uimarishaji wa mifumo ya utoaji ufaao wa mawasiliano na uwekaji wa mita za usambazaji wa kiwango cha umeme kinachotolewa ili kudhibiti hasara katika usambazaji. Hatua hizi zinatarajiwa kuongeza mapato ya shilingi milioni 200 kwa mwaka kwa kila asilimia ya hasara itakayopunguzwa.

## Kuimarishwa kwa Mtandao wa Usambazaji pamoja na kuimarishwa kwa ubora wa bidhaa

Kampuni imetambua na kuipa umuhimu miradi ya gharama ya takriban Dola 109 za Marekani ambayo inatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa usambazaji wa umeme ili kukidhi utashi wa bidhaa hiyo unaozidi kuongezeka. Benki ya Dunia imewasiliwa pamoja na mashirika mengine ya kifedha kugharamia miradi hiyo.

Pamoja na hayo, Kampuni ina mipango ya kupunguza kiwango cha utoaji cha sasa cha 11,000 kwa mwezi hadi 6,000 kufikia mwishoni mwa kipindi cha mwaka 2003/04 na kufikia



kiwango cha 3,000 kwa mwezi katika kipindi cha mwaka 2004/05. Hatua hizo kitaafikiwa kupitia uimarishaji wa nyaya za usambazaji na kubadilisha vifaa vilivyochakaa pamoja na milingoti isiyoweza tena kudhibiti usambazaji na ukaguzi wa mara kwa mara wa mtandao mzima wa usambazaji. Hatua hiyo itaongeza mapato kwa takriban Shilingi milioni 70 kwa mwaka.

## Kuimarishwa kwa misingi ya Huduma kwa Wateja

Kwa ajili ya kuimarisha mapato ya kimsingi, kuongeza upatikanaji wa faida na kuimarisha upatikanaji wa huduma za umeme katika taifa, Kampuni imejiandaa kulenga utoaji wa huduma za umeme kwa kiwango cha chini cha wateja wapya 150,000 kwa mwaka katika kipindi cha miaka 4 ijayo. Hii inalinganishwa na kuongezeka kwa kadiri kwa wateja 40,000 kwa mwaka kama ilivyoweza kufanyika katika kipindi cha miaka mitatu iliyopi-

ta. Kutokana na lengo hilo, Kampuni imepanga upya mikakati yake ya uunganishaji wa huduma ili kuimarisha uunganishaji kwa wateja wapya na pia kuhimiza uunganishaji wa makundi katika hali ya kupunguza gharama za uunganishaji kwa mtu mmoja mmoja. Kampuni inatafuta ufadhili wa kifedha kutoka kwa Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo Afrika Mashariki, na wafadhili wengine kwa ajili ya kutimiza lengo hilo. Mipango hiyo ya kuimarisha huduma kwa wateja inatarajiwa kuongeza kwa kadiri kiasi cha ziada cha mapato cha shilingi milioni 900 kwa mwaka.

## Kuimarishwa Uwezo wa Utoaji wa Umeme

Kuna utoaji wa kutosha wa nguvu za umeme kuukidhi utashi uliopo.

Kiwango cha juu zaidi cha utashi wa kila siku uliokuwepo katika kipindi hiki cha mwaka kilikuwa Mega-wati 785 MW ikilinganishwa na kiwango cha



Enhancing customer education and public awareness at the Nairobi ASK Show



*Final checks on electrical equipment before installation*

Mega-wati 760 mwaka uliotangulia. Utashi wa sasa ni Mega-wati 815. Kutokana na kiwango cha kuridhisha cha maji katika vituo vya utoaji umeme kutokana na nguvu za maji pamoja na kuwepo kwa kiwanda cha utoaji wa umeme kutokana na nguvu za joto.

Uwezo wa utoaji ulikuwa Mega-wati 1,051 katika mfumo uliunganishwa wa utoaji wa kawi kwa ajili ya kuukidhi utaji wa nguvu za umeme na hivyo kubakisha kiwango cha asilimia 34 cha umeme kilichowekwa akiba.

Kufuatia makubaliano yaliyoafikiwa mnamo 1996 kati ya serikali ya Kenya, Benki ya Dunia na washirika wengine wa maendeleo, Serikali ilijitokeza kuimarisha upya sekta ndogo ya utoaji wa umeme kupitia ushirikishaji wa sekta ya watu binafsi katika ustawishaji wa miradi ya utoaji kupitia mashindano katika sekta hiyo ndogo.

Kufungamana na hayo Kampuni yenu ililingia katika mikataba ya ununuzi wa umeme kati yake na watoaji wanne huru wa umeme ambao ni Iberafrica Power E.A. Limited (Mega-wati 56), Westmont Power Kenya Limited (Mega-wati 44), Tsavo Power Company Limited (Mega-wati 74) na OrPower4 Inc. (Mega-wati 48). Ingawa watoaji hao wamechangia pakubwa katika kupunguzwa kwa utoaji wa umeme gharama ya umeme kutoka vituo vyao imekuwa kubwa kutokana na gharama zao za mtaji wa

uwekezaji pamoja na uwezekano mkubwa wa kupata hasara.

Mashauriano na watoaji wengine wakubwa yanaendelea kwa lengo la kupunguza viwango vya ushuru.


Kama sehemu ya kutoa huduma za umeme ambazo wananchi wataweza kuzimudu, serikali imeelezea kujitolea kwake katika kuisaidia Kampuni ya Kenya Electricity Generation Company Ltd (KenGen) ili kutumia rasilimali za gharama nafuu katika uimarishaji wa siku zijazo wa utoaji wa nguvu za umeme. Uwezo mkubwa wa Kenya katika utoaji wa umeme kupitia nguvu za ardhi unaokisiwa kuwa Mega-wati 2000MW umewekwa katika orodha ya utoaji huo usiokuwa wa gharama ya juu kwa ajili ya nchi hii. Vile vile Serikali imeelezea kujitolea kwake katika kuisaidia Kampuni hiyo ya KenGen katika ustawishaji wa rasilimali za utoaji wa umeme kutokana na nguvu za ardhi kwa ajili

ya ulimarishaji wa vituo hivyo vya umeme kwa utoaji wa kawi hiyo kwa siku zijazo.

#### **Mifumo mipya ya Kifedha**

Kutokana na hasara ya kifedha kati ka Kampuni hii iliyosababishwa na hali ya ukame iliyoikumba nchi hii kutoka mwaka wa 1999 hadi mapema mwaka wa 2001 na kupelekea kutolewa kwa huduma za umeme kwa mgawo, Kampuni hii ilikuwa ikidaiwa na Kampuni ya KenGen kiasi cha Shilingi milioni 12,260 huku Serikali ikidai kiasi cha Shilingi milioni 3,639 kufikia tarehe 30 Juni, 2003. Serikali, Kampuni ya KenGen na Kampuni hii imekubaliana kuhusu hatua ambazo zitaimarisha msingi wa mtaji wa Kampuni hii pamoja na utoaji wa fedha zinazohitajika wakati wa kipindi cha ufufuzi. Hatua hizo ambazo zimeidhinishwa na Baraza la Mawaziri ni:

- (i) idhinisho rasmi la msamaha kutoka kwa Kampuni ya KenGen katika ulipaji wa kuchelewa wa fidia za riba wa Shilingi milioni 1,182 kutokana na deni lililopita muda wake wa kulipwa katika kipindi cha mwaka 2001/02. Msahama huo uliidhinishwa rasmi na serikali mnamo Octoba, 2002 na kuwekwa katika akaunti za Kampuni za kipindi cha mwaka 2001/02; na
- (ii) ikisubiriwa idhinisho kutoka kwa washika dau na Mamlaka inayosi-mamia masoko ya Hisa, kugeuzwa



kwa deni la Kampuni ya KenGen la Shilingi milioni 12,280 kuwa asilimia 7.85 ya hisa zisizokuwa za malimbikizi zinazoweza kununuliwa tena kwa malipo nafuu.

Kiwango hicho cha asilimia 7.85 kilichoafikiwa kufuatia uchunguzi wa kitaalamu uliofanywa na Dyer & Blair Investment Bank Ltd, kitapunguzwa ama kuongezwa katika kipindi cha 2009/2010 kwa mujibu wa kanuni za soko za wakati huo.

Deni la Shilingi milioni 3,639 linalodaiwa Kampuni hii ya KPLC na Hazina Kuu ya Serikali kama idhinisho hilo likipatikana pia litageuzwa kuwa hizo hizo za malipo nafuu katika misingi ya haki na manufaa kama ile iliyowekewa Kampuni ya KenGen. Hata hivyo hisa hizo hazitapewa haki ya kupigiwa kura.


Hata hivyo hizo kuhusu madeni hayo zitaiwezesha Kampuni hii kuweka akiba ya takriban Shilingi bilioni moja nutka moja katika makato ya riba kwa mwaka.

### UIMARISHAJI MPYA WA SEKTA NDOGO YA UTOAJI WA UMEME

#### Ubinafisishaji wa biashara ya umeme

Kampuni ya kitaifa ya utafiti wa kiuchumi ya Uingereza (NERA) iliyoteuliwa na serikali ilikamiliisha utafiti wake wa kuhusu mfumo wa soko na ubinafisishaji uliokusudiwa uimarishaji wa sekta hii ndogo.

Taarifa hiyo ilijadiliwa na washika dau mnamo mwezi Juni 2003 na taar-



ifa ya amwisho iliyo na maoni ya washika dau inatarajiwa kukamilishwa kufikia mwezi Desemba 2003.

Uunganishaji na Mtandao wa Kusini mwa Afrika wa utoaji wa Umeme (SAPP)

Kama ilivyotangazwa katika kipindi cha mwaka kilichopita, Serikali za Kenya, Tanzania na Zambia zina mpango wa kutekeleza mradi wa uunganishaji wa mataifa hayo matafu.

Mradi huo ukishatekelezwa utaiwezesha Kenya kuagiza nguvu za umeme kutoka kwa mtandao wa utoaji wa umeme wa mataifa ya Kusini mwa Afrika (SAPP).

Utafiti ulifanywa kuhusu mtandao wa kilometa 250 kati ya Arusha na taarifa ya mwisho kutolewa mnamo mwezi Novemba 2002.

Wakati huo huo utafiti kuhusu mtandao wa kilometa 670 wa laini ya kV330 kati ya Pensulo huko Zambia na Mbeya Tanzania pamoja na uimarishaji wa utoaji huko Tanzania unaendelea kufanywa hivi sasa.

Serikali inachunguza uwezekano wa kutekeleza mradi huu ili kuwezesha ununuzi wa umeme kutoka kwa mtandao wa Kusini mwa Afrika.

### Hati ya Kitaifa ya Maongozi kuhusu Kawi


Hati mpya ya kitaifa kuhusu kawi inakaribia kukamiliishwa kupitia ushirikishaji wa wizara ya kawi.

Maongozi hayo yanatarajiwa kuleta mazingira bora zaidi ya kudhibitika kifedha na kisheria katika sekta hiyo ili kuwavutia wawekezaji wa kibinafsi, kupunguza gharama za miradi ya siku zijazo katika utoaji wa umeme, kuongeza utumizi wa rasilimali za kiasili za utoaji wa umeme na kuimarisha kwa kiwango kikubwa zaidi upatikanaji wa nguvu za umeme humu nchini.

### SHUGHULI ZA KIBIASHARA ZA KIMSINGI

#### Utoaji na Usambazaji

Utoaji na usambazaji katika misingi ya kuimarisha ubora wa huduma za kuaminika kwa wateja pamoja na kupunguza hasara zinazotokana na kuharibika kwa vifaa vya usambazaji ni miongoni mwa miradi iliyoshughulikiwa kwa kina katika kipindi hiki cha mwaka. Miradi hiyo ilikuwa ni pamoja na kurekebisha vifaa vilivyoharibika ikiwa ni pamoja na milingoti ya kupitishia nyaya za umeme, kurekebisha mitambo ya usambazaji na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vifaa muhimu.



Kama sehemu ya uimarishaji huo, vituo vifuatavyo vilishughulikiwa.

Rabai kv11, kituo kidogo cha Kikuyu, laini ya Mbaraki ya kv33, Parklands - Mtandao wa Cathedral wa kv66, Kituo cha Nairobi North cha kv 66, ambapo miradi hiyo ilikamilishwa katika kipindi hiki cha mwaka kwa gharama ya Shilingi milioni 168, Pamoja na hayo kazi ya ujenzi wa vituo vidogo vya Matasia na Cianda vya kv66/11 ilianza kwa gharama ya Shilingi milioni 266. Miradi hii ilikusudiwa kupunguza hasara za kiufundi katika maeneo ya Ngong/Ongata Rongai na Runda/ Kiambu / Githunguri mtawalia.

#### Maendeleo ya Usambazaji

Laini ya Kiambe -Nairobi kv220 pamoja na vituo vyake vidogo

Kazi ya utekelezaji wa laini hiyo pamoja na vituo vyake vidogo iliendelea kutekelezwa na Kampuni ya Kimataifa ya KEC ya India kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (EADB) kwa gharama ya Dola milioni 7.35. Mradi huo unatarajiwa kukamilishwa kufikia mwezi Desemba 2003. Utakapokamilika, mradi huo utaimarisha usambazaji wa umeme kutoka vituo vya mabwawa hadi Nairobi.

Laini ya Olkaria-Nairobi kv220 na vituo vyake vidogo

Laini hiyo ya kilometa 117 ya vituo viwili vya kv 220 pamoja na vituo vyake vidogo chini ya mradi wa

Olkaria II wa nguvu za ardhi ambao ulikuwa ukitekelezwa na Kampuni ya KenGen kwa niaba ya Kampuni yenu unatarajiwa kukamilishwa kufikia mwezi Desemba 2003. Sehemu ya laini ya kilometa 3 kati ya Olkaria I na Olkaria II ilikamilishwa na kuanzishwa mnamo mwezi Aprili 2003. Kampuni ya KEC ya India na Siemens AG ya Ujerumani zinajenga laini hizo na vituo vyake vidogo mtawalia kwa gharama ya takriban dola milioni 17.1. Laini hiyo ya Kv220 itasambaza umeme kutoka kwa mradi mpya wa umeme kutokana na nguvu za ardhi wa Olkaria II hadi katika kituo kidogo kipa cha Nairobi North cha MVA180MVA Kv220/66 na kisha kuunganishwa katika kituo kidogo cha Dandora cha kv 220/132kv.

#### Matatizo ya nafasi za utekelezaji

Utekelezaji wa miradi ya laini za Kiambere-Nairobi na Olkaria -Nairobi kv220 umetazitwa na matatizo ya kutotaa nafasi kwa urahisi miongoni mwa wenye ardhi kunakokusudiwa kupitia miradi hiyo. Hii ilisababisha kukwama kwa shughuli za utekelezaji na kuongezeka kwa gharama.

#### Huduma kwa Mteja

Katika juhudi zake za kuwaridhisha wateja wake kupitia kuwafikishia karibu zaidi wananchi huduma za umeme, Kampuni hii ilendelea kuambatanisha mfumo mpya ulioratibiwa chini ya kustawisha biashara za kimaeneo. Pamoja na hayo, vituo vya


Kampuni vilivyopo vya kulipia huduma za umeme na vile vinavyosimamiwa kwa niaba yetu na washirika wetu wa kibiashara kama vile Benki na Posta viliendelea kuimarishwa. Ofisi mpya za Kampuni ya za kuwahudumia wateja zilijengwa huko Molo na Naivasha katika kipindi hiki cha mwaka. Hii ilikusudiwa kuwahudumia wateja kwa njia bora zaidi na pia kudhibiti ukusanyaji wa mapato.

#### Kuimarisha Ongezeko la Wateja

Mipango ya kuimarisha ongezeko la wateja, uuzaji zaidi wa kawi na mapato mapato zaidi kupitia uimarishaji wa mbinu za soko na za kubuni wateja zaidi iliandaliwa na kutekelezwa. Utoaji wa maelezo kuhusu upatikanaji wa huduma kwa wateja wakusudiwa ulifanywa kupitia vijitabu vya maelezo vilivyosanifiwa upya pamoja na mabango kuhusu shughuli zetu na pia ushiriki wetu katika maonyesho ya Kilimo ya chama cha (ASK) miongoni mwa mbinu nyinginezo. Kampuni ina malengo ya kupata wateja wanya 150,000 kuanzia kipindi cha mwaka cha 2003/2004.

#### Uhusiano wa Umma

Kampuni ilendelea kudumisha uhusiano mwema na washirika wake pamoja na wateja wake kupitia njia tofauti tofauti zilizokusudiwa kutoa hamasisho la kuzielewa vizuri zaidi shughuli zake. Ujumbe tofauti tofauti kuhusu ulipaji wa bili, athari za wizi wa stima na matokeo yake, harakati za kumaliza ufisadi, usalama na utoaji bora zaidi wa huduma za umeme ulitolewa kupitia elimu ya umma na kampeni za matangazo. Pia habari zifaazo kuhusu sekta ya kawi na mashirika zilitolewa kupitia vipindi vya habari na makala maalumu katika vituo vya utangazaji, magazeti na machapisho ya vijikaratasi na vijitabu na pia katika nakala za bili za umeme na vibanda vya Kampuni hii katika maonyesho kama vile maonyesho mbalimbali ya chama cha ASK kote nchini.




## Usambazaji wa Umeme katika sehemu za Mashambani

Kampuni iliendelea kutekeleza mpango wa usambazaji wa umeme katika sehemu za mashambani (REP) kwa niaba ya serikali. Shilingi milioni 1,057 zilitumika kwa ajili hiyo katika kipindi hiki cha mwaka. Hii ilikuwa ni pamoja na shilingi milioni 902 zilizotumika katika awamu ya kwanza na ya pili ya miradi iliyodhaminiwa na Uhispaniaa na Shilingi milioni 44 za mkondo wa pili na wa tatu wa awamu ya kwanza ya miradi ya uimarishaji wa uuzaji wa bidhaa katika nchi za kigeni (Stabex). Hii ilipelekea upatikanaji wa mtaji wa malimbikizo ya utumizi tangu kuanzishwa kwa mpango huo mnamo 1973 hadi kufikia shilingi milioni 7,230. Shilingi milioni 955 zilikusanywa kutoka kwa mapato ya ushuru wa usambazaji wa umeme katika sehemu za mashambani katika kipindi hiki cha mwaka ikilinganishwa na shilingi milioni 889 zilizokusanywa mwaka uliotangulia.

Utekelezaji wa miradi 32 chini ya awamu ya kwanza ya mpango uliodhaminiwa na Uhispania wa kima cha Dola milioni 10.255 uliendelea kufanyika katika kipindi hiki cha mwaka.

Kufuatia utathmini wa mkondo wa kwanza wa awamu ya kwanza ya mpango wa usambazaji wa umeme katika viwanda vya kahawa katika sehemu za mashambani (COFREP), ambao ulidhaminiwa na hazina ya Stabex ya Jumuiya ya Ulaya pamoja



na kuchunguzwa upya kwa orodha ya awali ya miradi iliyokusudiwa kutekelezwa chini ya mpango huo, viwanda 51 kati ya viwanda 53 vilidhinishwa kupelekewa umeme chini ya mkondo wa pili na wa tatu wa miradi huo. Kazi ya usanifu, usoroveya na upatikanaji wa vifaa ilikamilishwa mwaka uliotanguliaa na kazi ya ujenzi ikaanza katika kipindi hiki cha mwaka.

Zabuni za kazi za ujenzi kwa ajili ya miradi iliyotambuliwa kuhusiana na usambazaji huo wa umeme chini ya miradi uliodhaminiwa na Ufaransa kwa gharama ya Sarafu Ulaya milioni 9.1 zilipokelewa na kuchunguzwa na kuidhinishwa katika kipindi hiki cha mwaka.

Kampuni ya ujenzi ya, M/s Alstom /ABB Consortium iliteuliwa kuwa mjenzi mkuu ambapo kazi ya ujenzi itaanza katika kipindi cha mwaka 2003/2004 wa matumizi ya fedha.

Idadi ya wateja chini ya mpango huo iliongezeka kwa asilimia 10 hadi wateja 87,175 ikilinganishwa na wateja 79,391 mwaka uliotangulia.


Kiasi cha umeme kilichouzwa kiliongezeka kwa asilimia 15 kutoka milioni 128 hadi milioni 147, huku mapato yaliyokusanywa yakiongezeka kwa asilimia 3 kutoka shilingi milioni 979 mwaka uliotangulia hadi shilingi milioni 1,006.

## Wafanyikazi

Kampuni iliendelea kuimarisha mtaji wa wafanyikazi katika kipindi hiki cha mwaka. Licha ya hatua za kudhibiti idadi ya wafanyikazi ambayo inatekelezwa kwa sasa, Kampuni ili-wapa mafunzo tofauti tofauti wafanyikazi hapa nchini na ng'ambo pia ili kuimarisha utoaji wa huduma miongoni mwa mengine ikiwa ni pamoja na kuimarisha uhamasishaji kuhusu kuyabadili matarajio ya mteja.

Kampuni iliendelea kuimarisha uhusiano mwema na wafanyikazi wake kupitia chama cha wafanyikazi wa shughuli za umeme (KETAWU). Kufungamana na hilo, mikutano ya pamoja kati ya Kampuni hii na chama hicho ilifanywa kwa ajili ya kudumisha uhusiano huo mwema kwa ajili ya maslahi kwa pande zote mbili.

Wakati wa kipindi hiki cha mwaka, Kampuni hii ilikuwa na jumla ya wafanyikazi 6,269 ikilinganishwa na wafanyikazi 6,423 mwaka uliotangulia wakiwemo walio na ajira za kudumu, walio chini ya kandarasi na vibarua. Wafanyikazi 154 waliacha kufanyia kazi Kampuni hii kupitia sababu za kawaida. Kufikia tarehe 30 Juni, 2003, kiwango cha wafanyikazi



kilikuwa 104 kwa moja ikilinganishwa na kiwango cha 91 kwa moja mwaka uliotangulia..

### **Huduma ya Teknolojia ya Habari na Mawasilii (ICT)**

Kampuni inatambua umuhimu wa mchango wa huduma hizo katika utekelezaji wa shughuli zake na kutoa huduma zisizokuwa za gharama ya juu sana kwa wateja wake pamoja na washika dau wengine.

Kuambatana na hilo, Kampuni hii iliendelea kudhibiti kuwepo kwa vifaa na mifumo ya hali ya juu ya huduma hizo za ICT.

Kutokana na uhaba wa rasilimali, uwekaji wa mifumo hiyo ulitekelezwa kwa gharama ya chini kupitia usaidizi mkubwa kutoka kwa wafanyikazi.

### **UJIMARISHAJI WA UWEZO KATIKA UTOAJI WA NGUVU ZA UMEME**

Mradi Huru wa Umeme Kutokana na Nguvu ardhi Wa Olkaria III wa Mega -wati 48

Mradi huo unastawishwa na Kampuni ya OrPower4 Inc chini ya mpango wa kujisimamia mwenyewe wa makubaliano ya ununuzi wa umeme uliotelewa saina kati ya Kampuni hiyo na Kampuni ya KPLC mnamo mwezi Novemba 1998.

Awamu ya kwanza ya mradi huo ulio na uwezo wa kila kiwanda kutoa Mega- wati 8 ulizinduliwa mwezi Julai 2000 kisha nyongeza ya utoaji wa Mega-wati 4 ikapatikana mwezi Desemba 2000. Mashauriano na Kampuni ya OrPower 4 Inc. yanaendelea kwa ajili ya kutayarisha awamu ya pili ya mradi huo kwa uwezo wa kutoa Mega- wati 36,na inatarajiwa utazinduliwa na kuanza kufanya kazi kibiasharaa mnamo mwaka wa 2005.

Ujenzi wa laini ya kV 220 kuunganisha kituo hicho na kituo kidogo cha Olkaria II utiendelea vyema.



*A sealed pay deal for unionisable employees*

### **Miradi ya Kampuni ya KenGen**

Mradi wa Olkaria wa Mega-wati II 64 za umeme unaotokana na nguvu za ardhi.

Mradi wa Olkaria wa Mega-wati II 64 wa umeme unaotokana na nguvu za ardhi ulianzishwa mnamo mwezi Novemba 2003. Mradi huu utatoa Mega-wati 64 zaidi za umeme katika kiwango kinachotolewa.

Mradi wa Sondu Miru wa kutoa Mega-wati 60 za umeme unaotokana na nguvu za maji. Kazi ya ujenzi wa mradi huo iliendelea kuathiriwa sana na kusimamishwa kwa fedha kutoka kwa wafadhili wa mradi huo kutokana na masuala ya kimazingira na kijamii ambayo yanashughulikiwa na washika dau wahusika.

Mradi huo unaambatanisha usambazaji wa umeme wa kilometa 50 za kV 132 za umeme kutoka kituo cha umeme hadi katika kituo kidogo cha Kisumu cha kV 132/33.

### **MTIZAMO WA SIKU ZIJAZO**

Tangu miaka minne iliyopita shughuli za kibiashara za kampuni yenu ziliathiriwa pakubwa kwa upande wa vifaa kutokana na uhaba wa uwezo wa kutosha wa utoaji, gharama ya juu ya huduma ya umeme na kuzorota kwa uchumi ambapo kiwango cha ukuaji wa pato la kitaifa GDP kilikuwa asilimia -0.3 mnamo mwaka wa 2000,asilimia 1.1 mnamo mwaka 2001 na asilimia 0.9 mnamo mwaka wa 2002.

Kwa sasa kuna utoaji wa kutosha wa umeme kumudu utashi uliopo sasa huku utekelezaji wa miradi iliyoanzishwa ya utoaji wa umeme ukitegemewa kumudu utashi wa umeme wa siku zijazo. Kutokana na kuanza kuonyesha matokeo bora kwa hatua zilizochukuliwa, pamoja na matarajio ya kukwamuka kwa uchumi ambapo pato la taifa GDP linatarajiwa kukua kwa asilimia 1.4 mnamo mwaka wa 2003, wakurugenzi wana matumaini kuhusu malengo ya kampuni yenu ya kurejea katika utengezaji wa faida katika mwaka wa sasa wa matumizi ya fedha.

### **MWISHO**

Ningependa kuwashukuru wana-Halmashauri wenzangu pamoja na wafanyikazi kutokana na juhudi zao na kujitolea kazini kutekeleza harakati zetu za kujikwamua wakati Kampuni yetu ilipokuwa ikitekeleza shughuli zake chini ya mikabala migumu. Kwa niaba ya Halmashauri yenu, ningependa pia kuishukuru Serikali na Kampuni tanzu ya KenGen kutokana na usaidizi mkubwa kwa Kampuni yenu katika shughuli zake za mwaka,ambao utasaidia katika harakati za ufufuzi.

**MHANDISI ALFRED SAMBU**

*MWENYEKITI*

# REPORT OF THE DIRECTORS

The directors submit their report together with the audited financial statements for the year ended 30 June 2003.

## ACTIVITIES

The core business of the Company continues to be the transmission, distribution and retail of electricity purchased in bulk from Kenya Electricity Generating Company Limited (KenGen), Independent Power Producers (IPPs) and Uganda Electricity Transmission Company Limited (UETCL).

Appointments	Date
J O Oduor	5 February 2003
P Nyoike (Alternate M Nganga)	5 February 2003
J Magari (Alternate S Kitungu)	5 February 2003
A Sambu	28 March 2003
E Wasunna	8 April 2003
N Kiuna	8 April 2003
S Imu	8 April 2003
S Musyoka	8 April 2003

## RESULTS

	Sh'000
Loss before taxation	4,112,193
Taxation credit	(1,214,917)
Net loss for the year transferred to revenue reserve	<u>2,897,276</u>

## DIVIDENDS

A dividend of Sh 1,930,000 payable on the cumulative preference shares has been recognised in the income statement as finance costs. The directors do not recommend payment of a dividend on the ordinary shares in respect of the year.

In accordance with Article 128 of the Articles of Association of the Company, Messrs. A Sambu, J Magari, P Nyoike, E Wasunna, S Imu, N Kiuna and S Musyoka retire and, being eligible, offer themselves for election.

In accordance with Regulation 120 of the Articles of Association of the Company, T D Owuor retires by rotation and, being eligible, offers himself for re-election.

## CAPITAL EXPENDITURE

During the year, a total of Sh 1,667 million was spent on property and equipment. Capital contributions received from customers amounted to Sh 435 million resulting in a net capital cost to the company of Sh 1,232 million. Net capital work-in progress as at 30 June 2003 amounted to Sh 3,369 million compared to Sh 3,341 million in the previous year.

## AUDITORS

The responsibility for auditing the Company's books of account reverted to the Controller and Auditor General in accordance with Section II of the State Corporation Act, as amended by the Statute Law (Miscellaneous Law Amendments Act), 2002. The audit will subsequently be undertaken by the Controller and Auditor General or an audit firm nominated by him under Section 29(1)(b) of the Exchequer and Audit Act.

Deloitte & Touche were nominated by the Controller and Auditor General to carry out the audit for the year ended 30 June 2003.

## DIRECTORS

The present members of the board of directors are shown on page 2 and changes since last year are as follows:

Resignations	Date
S Gichuru	5 February 2003
J Kinyua (Alternate P Gakuru)	5 February 2003
W M Mwangi (Alternate B M Nzioki)	5 February 2003
D Afande	28 March 2003
S O J Ambundo	8 April 2003

## BY ORDER OF THE BOARD

Laurencia K Njagi (Mrs)  
Secretary  
Nairobi  
24th November 2003

# TAARIFA YA WAKURUGENZI

Wakurugenzi wanawasilisha taarifa yao pamoja na taarifa za ukaguzi wa kifedha kwa kipindi cha mwaka kilichomalizika tarehe 30 Juni 2003.

## SHUGHULI

Shughuli ya kimsingi ya Kampuni inaendelea kubakia kuwa utoaji, usambazaji na uuzaji wa umeme kwa kiwango kikubwa kutoka Kampuni ya (KenGen), watoaji wengine huru wa umeme (IPPs) na Kampuni ya utoaji wa Umeme ya Uganda (UETCL).

## MATOKEO

	Sh'000
Hasara kabla ushuru	4,112,193
Mkopo wa ushuru	(1,214,917)
Kiwango cha jumla cha hasara kilichogeuzwa kuwa akiba ya mapato	2,897,276

## MGAO WA HISA

Mgao wa hisa wa Shilingi 1,930,000 zinazoweza kulipwa katika hisa za malimbikizi umetambuliwa kama gharama za kifedha katika taarifa ya mapato. Wakurugenzi hawapendekezi mgao wa hisa wa hisa za kawaida za kipindi hiki cha mwaka.

## MATUMIZI YA MTAJI

Wakati wa kipindi hiki cha mwaka, jumla ya shilingi milioni 1,667 zilitumika katika ununuzi wa mali na vifaa.

Michango ya mtaji kutoka kwa wateja ilifikia Shilingi milioni 435 katika jumla ya gharama ya mtaji kwa Kampuni ya kima cha Shilingi milioni 1,232. Kiwango cha jumla cha mtaji kilichokuwa kikitumika kufikia tarehe 30 Juni 2003 kilikuwa ni Shilingi milioni 3,369 ikilinganishwa na kiwango cha Shilingi milioni 3,341 mwaka uliotangulia.

## WAKURUGENZI

Wanachama wa sasa wa Halmashauri ya wakurugenzi wameorodheshwa katika ukrasa wa pili huku mabadiliko tangu mwaka uliopita ikiwa ni kama ifuatavyo:

Waliostaafu	Tarehe
S Gichuru	5 Februari 2003
J Kinyua (Mwakilishi - P Gakunu)	5 Februari 2003
W M Mwangi (Mwakilishi - B M Nzioki)	5 Februari 2003
D Afande	28 Machi 2003
S O J Ambundo	8 Aprili 2003

Walioteuliwa	Tarehe
J O Oduor	5 Februari 2003
P Nyoike (Mwakilishi - M Nganga)	5 Februari 2003
J Magari (Mwakilishi - S Kitungu)	5 Februari 2003
A Sambu	28 Machi 2003
E Wasunna	8 Aprili 2003
N Kiuna	8 Aprili 2003
S Imu	8 Aprili 2003
S Musyoka	8 Aprili 2003

Kwa mujibu wa Kifungu cha sheria za Kampuni nambari 128, A Sambu, J Magari, P Nyoike, E Wasunna, S Imu, N Kiuna na S Musyoka wanastaafu na kwa kutimu kwao wanagombea tena uchaguzi.

Kwa mujibu wa sehemu nambari 120 ya sheria za Kampuni, T D Owor anastaafu kwa zamu na kutokana na kutimu kwake anagombea tena uchaguzi.

## WAKAGUZI WA FEDHA

Wajibu wa kukagua vitabu vya fedha vya Kampuni uliwekwa tena chini ya Msimamizi na Mkaguzi mkuu wa fedha kwa mujibu wa sehemu II ya sheria za Mashirika ya Umma kama ilivyofanyiwa marekebisha mnamo 2002. Ukaguzi wa fedha utafanywa na Msimamizi na Mkaguzi mkuu wa Fedha au Kampuni ya ukaguzi wa Fedha aliyoteua chini ya sehemu 29(1)(b) ya sheria za Hazina Kuu ya Serikali na ukaguzi wa fedha.

Kampuni ya Deloitte & Touche iliteuliwa na Msimamizi na Mkaguzi Mkuu wa fedha kufanya ukaguzi wa fedha kwa kipindi cha mwaka kilichomalizika tarehe 30 Juni 2003.

## CHINI YA AGIZO LA HALMASHAURI

Bi. Laurencia K Njagi  
 Katibu  
 Nairobi  
 24th November 2003

# STATEMENT OF DIRECTORS' RESPONSIBILITIES TAARIFA YA MAJUKUMU YA WAKURUGENZI

## STATEMENT OF DIRECTORS' RESPONSIBILITIES

The Companies Act requires the directors to prepare financial statements for each financial year which give a true and fair view of the state of affairs of the Company as at the end of the financial year and of the operating results of the Company for that year. It also requires the directors to ensure the Company keeps proper accounting records which disclose with reasonable accuracy at any time the financial position of the Company. They are also responsible for safeguarding the assets of the Company.

The directors accept responsibility for the annual financial statements, which have been prepared using appropriate accounting policies supported by reasonable and prudent judgements and estimates, in conformity with International Financial Reporting Standards and in the manner required by the Companies Act. The directors are of the opinion that the financial statements give a true and fair view of the state of the financial affairs of the Company and of its operating results. The directors further accept responsibility for the maintenance of accounting records which may be relied upon in the preparation of financial statements, as well as adequate systems of internal financial control.

Nothing has come to the attention of the directors to indicate that the Company will not remain a going concern for at least the next twelve months from the date of this statement.

Eng. Alfred W Sambu

Eng. Jasper O Oduor

} Directors

28th October, 2003

## TAARIFA YA MAJUKUMU YA WAKURUGENZI

Sheria ya Kampuni inawataka wakurugenzi kutayarisha taarifa za kifedha kila mwaka wa matumizi ya fedha ambazo zitaonyesha uhalisi wa hali ya shughuli za Kampuni kufikia mwishoni mwa mwaka wa matumizi ya fedha na pia matokeo ya shughuli za tendakazi za Kampuni kwa kipindi hicho cha mwaka.

Pia wakurugenzi wanatakiwa kuweka taarifa za ukaguzi wa kifedha ambazo zinaonyesha kwa uhakika hali ya kifedha ya Kampuni. Pia wanawajibika kullinda mali ya Kampuni.

Wakurugenzi hukubali jukumu la taarifa za kifedha za mwaka ambazo zimetayarishwa kupitia maongozi ya uhasibu yafaayo kwa misingi ya makadirio yaliyo na uamuzi wa uhakika kulingana na viwango vya kimataifa vya utoaji wa taarifa za kifedha na pia katika hali ya kuzingatia sheria za Kampuni. Ni maoni ya wakurugenzi kwamba taarifa za kifedha zinaonyesha uhalisi wa hali ya kifedha ya Kampuni pamoja na matokeo ya shughuli zake. Zaidi ya hayo, wakurugenzi wanakubali jukumu la uhifadhi wa taarifa ambazo huenda zikategemewa katika utayarishaji wa taarifa za kifedha pamoja na kuwa na mifumo ya kutosha ya usimamizi wa ndani wa kifedha.

Hakuna kilichowafikia wakurugenzi kuonyesha kwamba Kampuni haitabakia kwa hali ilioko kutoka tarehe ya taarifa hii hadi miezi 12 ijayo.

# CORPORATE GOVERNANCE

## CORPORATE GOVERNANCE

Corporate Governance is the process and structure used to direct and manage business affairs of the Company towards enhancing prosperity and corporate accounting with the ultimate objective of realising shareholders long term value while taking into account the interest of other stakeholders.

The Company is committed to business integrity and professionalism in all its activities. As part of this commitment the Board fully supports issues articulated by the Capital Market Authority so as to bring the level of Governance in line with International trends.

We confirm that the Rules and Regulations as issued by both the Nairobi Stock Exchange (NSE) and the Capital Markets Authority (CMA) govern us.

## BOARD OF DIRECTORS

The Board of Directors has ten members comprising the Managing Director and nine non-executive directors, including the Chairman. All the non-executive directors are independent within the meaning of the Combined Code. The Board meets at least once a month or more often in accordance with requirements of the business.

The separate roles of the Chairman and Managing Director are acknowledged. The Chairman is primarily responsible for the running of the Board and ensuring that it is supplied, in a timely manner, with sufficient information to enable it to discharge its duties. The Managing Director is responsible for co-ordinating the running of the business and implementing corporate strategy. Agreed procedures are in place for all directors to receive appropriate training and to take independent professional advice if necessary. All the non-executive directors of the Board are independent of management and free from any business or other relationships which could materially interfere with the exercise of their independent judgement.

Further details of directors are given on page 2.

The Board meets at least once a month or more often in accordance with requirements of the business. It has a formal schedule of matters reserved to it, which include definition of corporate strategies, policy plans and objectives, review of monthly corporate performance, approval of quarterly, annual and interim results, annual budgets, disposals, and material agreements and commitments.

## DIRECTORS' REMUNERATION

Details of directors' remuneration are set out in the report on pages 42. There did not exist any arrangement to which

the Company is a party, whereby directors might acquire benefits by means of the acquisition of Company's shares. There were no directors' loans at any time during the year.

The Board has instituted the following Committees, which meet regularly under the terms of reference defined by the Board.

## AUDIT COMMITTEE

The Board constituted an Audit Committee in 1999. This committee meets at least three times a year and is chaired by a non-executive director. Its responsibilities include but are not limited to review of routine financial information, annual budgets, examination of quarterly, half year and annual financial statements, review of operations and major findings of the Internal Audit function and liaison with External Auditors.

## FINANCE AND REMUNERATION COMMITTEE

The Board has in place a fully operational Finance & Remuneration Committee whose mandate includes determining remuneration of the managing director and senior management staff, approval of recommendations for appointment of senior management staff, and recommending to the Board the remuneration of non executive directors.

## CENTRAL TENDER COMMITTEE

There is a Tender Committee established pursuant to the requirements of the Exchequer and Audit Act (Public Procurement Regulations), 2001, whose chief responsibilities include approval of award of tenders of goods and services with a value exceeding Shs.500,000, which meets twice monthly or when necessary. The members of this committee include the Managing Director and three non-executive directors. Other members are senior management staff as spelt out in the Procurement Regulations aforementioned.

## INTERNAL CONTROLS

The Company has systems and processes to ensure requisite controls, physical security of assets and reporting of accurate and up-to-date information. A comprehensive accounting system is also in place.

## ACCOUNTABILITY AND AUDIT

Directors' responsibilities in relation to financial statements  
The Company law requires the directors to prepare financial statements for each financial year which give a true and fair view of the state of affairs of the company as at the end of the financial year and of the profit or loss of

the Company for that period. The directors are responsible for ensuring that suitable accounting policies are consistently applied supported by reasonable and prudent judgements and estimates, and those applicable accounting standards are followed.

The directors have responsibility for ensuring that the Company keeps proper accounting records, which disclose with reasonable accuracy at any time the financial position of the Company and enable them to ensure that the financial statements comply with the Companies Act. They also have general responsibility for the systems of internal control for safeguarding the assets of the Company and to prevent and detect fraud and other irregularities.

#### COMMUNICATION WITH SHARE HOLDERS

The Company places great importance on communication with its shareholders and publishes in the local dailies its financial statements on half-year and annual basis. The full report and accounts are distributed to all shareholders each year. The Company also complies with obligations contained in Nairobi Stock Exchange's Listing Rules, Capital Markets Authority Act and Company Act.

#### MAJOR SHARE HOLDERS

The Company files with CMA and NSE a monthly report on the top 10 major shareholders.

These are as follows;

Name	No of Shares	%
1. Permanent Secretary to the Treasury	32,853,268	40.42
2. National Social Security Fund	8,553,168	10.81
3. Barclays (Kenya) Nominees Ltd.	4,275,007	5.40
4. Kestrel Capital Nominees Ltd	3,256,574	4.12
5. Jubilee Insurance Co. Ltd	1,937,029	2.45
6. UAP Provincial Insurance Ltd.	1,726,547	2.18
7. Apollo Insurance Co. Ltd.	1,365,659	1.73
8. Co-operative Bank of Kenya Ltd.	1,221,757	1.54
9. Khetshi Dharamshi & Company Ltd	1,074,879	1.35
10. Paul Wanderi	1,058,600	1.24

# MWONGOZO WA MASHIRIKA

## MWONGOZO WA MASHIRIKA

Usimamizi wa mashirika ni mfumo na utaratibu unaotumiwa kuongoza na kusimamia masuala ya kibiashara ya Kampuni kwa lengo la kuimarisha ustawi na uhasibu wa mashirika ili kudumisha thamani ya muda mrefu ya washika dau huku yakizingatiwa maslahi ya washika dau wengine.

Kampuni inazingatia uadilifu wa kibiashara na utaalamu katika shughuli zake zote.

Kwa mazingatio hayo Halmashauri inaunga mkono kikamilifu masuala yaliyoelezewa na Mamlaka ya Masoko ya Hisa katika kuleta kiwango cha usimamizi unaoambatana na viwango vya kimataifa.

